

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA SITINI

5 JULAI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA SITINI TAREHE 5 JULAI, 2017

I. DUA

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua saa 3:00 asubuhi na kuliongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndg. Laurance Makigi
2. Ndg. Neema Msangi

II. TAARIFA YA SPIKA

Naibu Spika alitoa taarifa kuhusu Miswada ya Sheria zilizopata kibali cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Sheria. Miswada hiyo ni:-

1. Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Mwaka, 2017 (*The Appropriation Bill, 2017*); na
2. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Bill, 2017*).

Miswada hiyo sasa inaitwa:-

1. Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Na. 3 ya Mwaka, 2017 (*The Appropriation Bill, 2017*); na
2. Sheria ya Fedha Na. 4 ya Mwaka 2017 (*The Finance Act, No. 4 of 2017*).

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha Mezani Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

Mhe. Joram Ismael Hongoli aliwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti Wa Kamati ya Katiba na Sheria Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

Mhe. Masoud Abdallah Salim aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

IV. MASWALI

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 497: Mhe. Boniphace Mwita Getere

Nyongeza: Mhe. Boniphace Mwita Getere

Swali Na. 498: Mhe. Catherine Nyakao Ruge (kny: Mhe. Esther Nicholas Matiko)

Nyongeza: Mhe. Catherine Nyakao Ruge

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali na. 499: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

Nyongeza: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

TANGAZO LA DHARURA

Naibu Spika aliwatangazia Wabunge wa Kamati inayoshughulikia Madini ya Tanzanite kuwa wamwone Mhe. Dotto Mashaka Biteko kwa ajili ya Kikao cha Dharura.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Swali Na. 500: Mhe. Stella Ikupa Alex

Nyongeza: Mhe. Stella Ikupa Alex

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na. 501: Mhe. James Francis Mbatia (Kny: Mhe. Ally Saleh Ally)

Nyongeza: Mhe. James Francis Mbatia

V. MATANGAZO

1. Wageni 27 wa Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao ni Wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kutoka *Mzizima Savings and Credit Cooperation Union (MSACCU)*.
2. Wageni 30 wa Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Viongozi pamoja na Wachezaji wa Timu ya Singida United FC kutoka Mkoani Singida.

3. Wageni 54 wa Mhe. Felister Aloyce Bura waliotembelea Bunge ambao ni Wanafunzi 49 wa Darasa la Saba na Walimu 5 wa Shule ya Msingi Tumaini iliyoko Kata ya Nkuhungu, Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoani Dodoma.
4. Wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba, Muhimbili kutoka Jijini Dar es Salaam, wapo Mkoani Dodoma kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika Hospitali ya Milembe.

VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*]. – **ULISOMWA MARA YA PILI.**

1. Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017.
2. Mhe. Mohamedi Omary Mchengerwa, Mwenyekiti wa Katiba na Sheria aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017.
3. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mhe. Hamidu Hassan Bobali.

TANGAZO

- Wageni 4 wa Mhe. Shabani Omari Shekilindi kutoka Lushoto ambao ni Wanamazingira (Friends of Usambara).
- Wageni 2 wa Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka wakiongozwa na Zuberi Mewile.
- Taarifa ya Msiba wa Ndg. Tonya Kandielo aliyekuwa Mkurugenzi wa *African Development Bank*, na kuwezesha upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa Taifa la Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa Barabara, amefariki Dunia, hivyo Wabunge wote wanaombwa na

Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Hazina Dodoma kuweza kusaini Kitabu cha Maombolezo na Rambirambi.

- Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*], kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Joseph Kizito Mhagama	-	CCM
2. Mhe. Selemani Jumanne Zedi	-	CCM
3. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara	-	CHADEMA
4. Mhe. Riziki Shahari Mngwali	-	CUF
5. Mhe. Joram Ismael Hongoli	-	CCM
6. Mhe. Richard Phillip Mbogo	-	CCM
7. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi	-	CHADEMA
8. Mwanasheria Mkuu wa Serikali		

VII. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*] kulikuwa na marekebisho yafuatayo:-

- Kabla ya neno NOTICE katika ukurasa wa 1 kumeingizwa Arrangements of Sections.
- Mhe. Waitara alikuwa na Amendments kuanzia Ibara ya 3, 4, 5, 6, 7, 10 na 11 ambazo aliziondoa mwenyewe.
- Ibara ya 11 na 15 zilikuwa na mabadiliko ya Serikali
- Ibara nyingine zote zilizobakia zilipita bila marekebisho yoyote ambapo Muswada ulikuwa na Ibara 15 tu.

VIII. BUNGE LILIREJEA

Bunge lilirejea na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa hoja ili Muswada huo ukubaliwe na Bunge baada ya Hatua zote za kusomwa Mara ya Kwanza na Pili.

- Hoja ilitolewa na kuafikiwa
- Muswada wa Sheria ya Serikali ulipitishwa na Bunge na **KUSOMWA MARA YA TATU.**

IX. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah alitoa taarifa kwa Bunge kuwa Bunge limemaliza shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti wa Bunge la 11.

X. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa alisoma Hotuba ya kuahirisha Bunge.

WARAKA WA SPIKA

- Kuhusu kuundwa Kamati Teule ya Uchunguzi wa Madini ya Almasi iliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Rais kuhusu Uchunguzi wa Makinikia.
- Hadidu za Rejea kuhusu Kamati hiyo zilihusu uchimbaji, usimamizi na uwekezaji wa Madini hayo.
- Kituo cha kazi cha Kamati hiyo ni Dodoma na Sekretarieti itaundwa kusaidia Kamati.

Wajumbe wa Kamati hiyo ni:-

- | | | |
|--------------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi | - | CHADEMA |
| 2. Mhe. Shally Joseph Raymond | - | CCM |

- | | | |
|------------------------------------|---|------------|
| 3. Mhe. Rashid Ali Abdallah | - | CUF |
| 4. Mhe. Allan Joseph Kiula | - | CCM |
| 5. Mhe. Taska Restituta Mbogo | - | CCM |
| 6. Mhe. Riziki Shahari Mngwali | - | CUF |
| 7. Mhe. Richard Mganga Ndassa | - | CCM |
| 8. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | - | CCM |
| 9. Mhe. Mussa Azzan Zungu | - | Mwenyekiti |

XI. WIMBO WA TAIFA

Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa kwa kuahirisha Bunge.

XII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 6:45 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Jumanne tarehe 5 Septemba, 2017 saa 3:00 asubuhi.